**0756 520 521/ 0783 876 328**

**JINA LA MWANAFUNZI ____________________________________________**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Ubetu Mawenzi. Shule ni ya mchanganyiko (wavulana na wasichana) na ni ya bweni. Shule iko umbali wa kilometa moja kutoka eneo la Mashima madukani.

Shule ya Sekondari Ubetu Mawenzi ni shule yenye nidhamu ya hali ya juu na inafanya vizuri kitaaluma

Shule ya Sekondari Ubetu Mawenzi ni shule ya sayansi ndiyo maana watoto wetu wengi wanaohitimu kidato cha nne wanapoenda Kidato cha tano wanasoma masomo ya sayansi.

Ubetu mawenzi Sekondari inatoa huduma bora kwa wanafunzi kwa kuwa ina walimu waliohitimu vizuri sana na watumishi wengineo wapo wenye sifa stahiki.

Unatakiwa kuripoti tarehe ________________________. Tunakutakia kila la heri unapojiandaa kujiunga nasi.

WAKO MWAMINIFU

JAPHET MUIA

MKURUGENZI.

| NA | KIFAA | WEKA ALAMA YA VEMA(V) | KWA MATUMIZI YA OFISI |
|---|---|---|---|
| 1. | Madaftari makubwa 12 (4 quire) | | |
| 2. | Four figure mathematical table | | |
| 3. | Mkebe wa Hisabati (OXFORD) | | |
| 4. | Mafaili 2 ya plastiki (spring file) | | |
| 5. | Rimu mbili za karatasi nyeupe za kompyuta | | |
| 6. | Dictionary na kamusi ya kiswahili | | |
| 7. | Kadi ya Bima ya Afya | | |
| 8 | kitabu cha matokeao (Report book) | | |
| 9 | Kitambulisho cha shule (vinapatikana shuleni) | | |
| 10. | Barua ya kujiunga shule. Matokeo ya mtihani wa Taifa. (NECTA) | | |
| 11. | SARE YA SHULE<br>**Wavulana**: Suruali nyeusi na sweta nyekundu , shati jeupe ,mkanda mweusi na tai yenye mistari mieusi na mieupe.<br>**Wasichana**: Sketi nyeusi , tai nyeusi yenye mistari mieusi na mieupe,shati jeupe na soksi nyeupe.<br>**NB: SARE YA SHULE INAPATIKANA SHULENI.** | | |
| 12. | Taulo,ndala,sabuni,toilet paper,jaketi jeusi,rangi ya viatu,dawa ya meno na mswaki,pedi kwa wasichana na mahitaji mengine muhimu ya binafsi. | | |
| 13. | Shuka mbili za rangi ya bluu | | |
| 14. | Mablanketi 2 | | |
| 15. | Sahani ,kikombe na kijiko | | |
| 16. | Beseni (karai) na ndoo | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17. | Godoro na chandarua cha mbu chenye dawa | | |
| 18. | Jembe kwa wavulana | | |
| 19. | Panga kwa wasichana | | |
| 20. | Track suit nyeusi kwa watoto wa kiume(aweke alama)<br>Track suit ya blue kwa watoto wa kike (aweke alama) | | |

## KARO YA SHULE MWAKA 2024.

- Ada ya shule kwa mwaka wa masomo ni 1,600,000/=
- Ada yetu inalipwa kwa awamu nne.

## SARE YA SHULE

- Sare ya shule inapatikana hapa shuleni kwa gharama ya 200,000/=

Karo yote lazima ilipiwe AKAUNTI YA SHULE YA **CRDB**: **0150324980100**

JINA LA AKAUNTI: UBETU MAWENZI SECONDARY SCHOOL.

ANGALIZO:

- Gharama ya fomu ya kujiunga ni Tshs. **20,000**/= hii ni pamoja na gharama ya mtihani wa kujiunga.
- Malipo yote ya ada yafanyike benki. Kwa taarifa au malipo ya vitu vingine wasiliana na Mhasibu. 0764045723.

# SHERIA ZA SHULE

## MALENGO YA SHULE

a) Kuwezesha uendashaji rahisi na utulivu wa jumuiya ya shule

b) Kutoa maelekezo sahihi ya uendeshaji wa jumla wa shule

c) Kuwezesha wanafunzi kukaa na kuwa raia wa kutarajiwa,kutegemewa na kuwajibika.

## ORODHA YA SHERIA ZA SHULE

| SHERIA | ADHABU |
|---|---|
| Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti shuleni siku ya kufungua shule saa saba kamili. | Mwanafunzi ambaye hataripoti kwa wakati atatumwa nyumbani aje na mzazi. |
| Mwanafunzi anatakiwa aoneshe utii na heshima kwa walimu, viranja na wafanyakazi wote wa shule. | Mwanafunzi ambaye atavunja sheria hii atapata adhabu zifwatazo:<br>i) kutowatii viranja – adhabu isiyopungua masaa mawili<br>ii) kutowatii walimu na wafanyakazi – atatumwa nyumbani kwa likizo isiyopungua siku tano. |
| Ratiba yote ifwatwe | Mwanafunzi atakayevunja sheria hii,atachapwa viboko vinne |
| Mwanafunzi ajiheshimu na kuheshimu wenzake. | Atakayepigana- atatumwa nyumbani kwa kipindi cha wiki mbili.<br>Na kisha atachapwa viboke visivyozidi 4. |
| Mwanafunzi asizungumze lugha nyingine tofauti na kingereza. | Adhabu ya kufanya kazi za nje kwa muda wa masaa 2. |
| Nguo za nyumbani,mikufu , kofia ,hereni,rangi za kucha na midomo na mavazi mengine yote ambayo si sare ya shule hayaruhusiwi. | Mwanafunzi atakayepatakina na mavazi au vipodozi atapewa adhabu kazi za nje kwa muda usiopungua masaa 4 kisha atalazimika kuteketeza nguo hizo na vipodozi. |
| Vifaa vya kielektroniki haviruhusiwi kwa mfano:simu,lani za simu, kamera n.k. | Atakayepatikana nazo atatumwa nyumbani kwa likizo ya wiki mbili,simu hiyo itateketezwa au kutumbukizwa majini. |

| | |
|---|---|
| Utoro ni marufuku | Mwanafunzi yeyote ambaye atatoka shuleni bila ruhusa ya mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule atasimamishwa masomo. |
| **<u>Sehemu zifwatazo ni marufuku kwa mwanafunzi</u>**<br>a) Ofisini<br>b) Maabara<br>c) Vyumba vya walimu<br>d) Uzio wa shule<br>e) lango kuu la kuingilia shuleni.<br>f) Jikoni<br>g) Mabweni | Mwanafunzi atakayeingia sehemu hizi bila ruhusa atatumwa nyumbani aje na mzazi na endapo kuna chochote ambacho kitakuwa kimepotea au kuharibiwa mwanafunzi huyu atakuwa mshukiwa mkuu. |
| Kutoka nje ya shule kwa shughuli maalum | Mwanafunzi atakayetoka nje ya shule bila kusindikizwa na mwalimu atasimamishwa masomo kwa kipindi cha wiki mbili. |
| Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na wageni bila ruhusa. | Atapewa adhabu ya kazi za nje isiyopungua masaa 3. |
| Mwanafunzi haruhusiwi kupeleka wageni mabwenini au darasani. | Atachapwa viboko vinne |
| Mwanafunzi haruhusiwii kushiriki ulevi wa aina yeyote mfano:<br>- Pombe<br>- Sigara<br>- Mirungi<br>- Madawa yote ya kulevya | Atakayehusika atasimamishwa masomo |
| Aina yeyote ya vyakula kutoka nje haviruhusiwi shuleni | Atakayeleta vyakula hivi atapewa adhabu ya kuvila vyote kabla ya kuingia shuleni kisha atapewa adhabu isiyopungua masaa 3. |
| Wizi ni marufuku | Atakayepatikana na kosa hili atasimamishwa masomo na kurejesha mali iliyoibiwa mara tano ya mali hio. |
| Mwanafunzi anapaswa kutunza mali ya shule | Atakayeharibu ataifidia na kupewa adhabu na kazi za nje isiyopungua masaa manne. |

| | |
|---|---|
| Mwanafunzi anapaswa kutunza na kuyaweka mazingira ya shule kuwa safi.<br>Mwanafunzi haruhusiwi kukanyaga maua na ukoka. | Atakayevunja sheria hii atadhibiwa viboko vitano. |
| Mwanafunzi anatakiwa kufanya kazi yeyote atakayopangiwa na viranja | Atakayevunja sheria hii ataadhibiwa kwa kupewa kazi za nje zisizozidi masaa manne. |
| Mwanafunzi anatakiwa kufanya mitihani yote | Atakayevunja sheria hii hataruhusiwa kupanda darasa. |
| Silaha kama:<br>a)Visu<br>b)Mambia<br>c) Sime<br>d) Mishale<br>e) Manati<br>ni marufuku. | Atakayepatikana na silaha hizi atachapwa viboko vinne na kutumwa nyumbani kwa likizo isiyopungua wiki mbili. |
| Urafiki wa kimapenzi ,uchumba,kuoa na kuolewa uwapo mwanafunzi hauruhusiwi. | Mwanafunzi atakayejihusisha na mambo haya ataachishwa masomo moja kwa moja. |
| Wastani wa shule ni asilimia 60. | Mwanafunzi ambaye hatafikia wastani huu hatapanda darasa. |
| Mwanafunzi haruhusiwi kuweka hela bwenini | Mwanafunzi ambaye atapatikana na hela bwenini atatumwa nyumbani kwa kipindi cha wiki moja |
| Vipindi vya dini – kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vya dini katika dhehebu lake | Mwanafunzi amabaye atakosa kuhudhuria vipindi vya dini mara tatu mfululizo bila sababu atapewa adhabu ya kazi za nje zisizopungua masaa mawili |

a. JINA LA MZAZI TAREHE SAINI

______________________________ __________ ____________

b. JINA LA MWANAFUNZI TAREHE SAINI

______________________________ ____________ __________

c. MKUU WA SHULE TAREHE SAINI

______________________________ ____________ __________

## **MAKOSA AMBAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE (EXPULSION)**

1. Kufanya tendo la ndoa
2. Ushoga
3. Kupigana
4. Kuharibu mali ya shule kimaksudi
5. Kuoa
6. Kutofikisha wastani wa 50% kwa mitihani mitatu mfululizo
7. Kukataa au kususia adhabu
8. Kuchelewa kufika shuleni bila kutoa taarifa
9. Kuongoza mgomo
10. Kujihusisha na mgomo
11. Kutukana kwa maandishi ya ukutani,ubaoni au kwenye madawati
12. Kutokula chakula kinachopikwa shuleni
13. Uchochezi wa aina yeyote
14. Wizi
15. Kutoka nje ya shule bila ruhusa

SHULE YA SEKONDARI UBETU MAWENZI

S.L.P 66,

TARAKEA-ROMBO.

**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI**

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

JINA: ____________________________________________

NAMBARI YA KUJIANDIKISHA____________________________

JINSIA ____________________________________________

TAREHE YA KUZALIWA__________________________________

ANWANI YA KUDUMU YA NYUMBANI ________________________

WILAYA__________________TARAFA______________________

KATA______________________KITONGOJI_________________

ALAMA ZA MTIHANI WA TAIFA (NECTA) ____________________

NAMBAYA MTIHANI____________________________________

PREM NUMBER YA MWANAFUNZI __________________________

MWAKA ALIYOFANYA MTIHANI ___________________________

SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA___________________________

SHULE UNAYOTOKA (KAMA UNAHAMA)_____________________

SAHIHI YA MWANAFUNZI________________TAREHE______________

TAARIFA YA MZAZI /MLEZI

JINA LA MZAZI/MLEZI_________________________________

NAMBA YA SIMU______________________________________

ANWANI YA KUDUMU___________________________________

KAZI________________________________________________

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI__________________TAREHE____________

**RE: <u>STUDENT MEDICAL FORM</u>**

Kindly examine the bearer of this form on the following and advise us accordingly.

Name of the students …………………………………….…………………………………………

**A.** RECOMMENDED TESTS

1. B/S

   :Results…………………………………………..……………………………..………

2. Stool :Results………………………………………………………………………………

3. Widal Test

   :Results ……………………..……………………………………………………………

4. Urinalysis

   :Results ……………………………………………………………..………………………

5. Vision ability (eyes)

   :Results……………………………………………………..……..……………………………

6. Hepertitis

   :Results…………………………………….………………………………………….……

7. Abdomen :Results…………………………………………………..…………………………

8. HIV(AIDS)

   :Results……………………………………...……………………………………………

9. Skin :Results…………………………..………………………………………………

10. TB :Results…………………………………………………………………………………

11. Ears

    :Results…………………………………..……………………………………………

12. HB

    :Results……………………………………………………………………………………..

13. Allergies :Results……………………….…………………..………………………………

14. Syphilis test

    :Results…………………………………………...…………………………………………

15. Teeth

    :Results………………………………………………...……………………………………

16. E.N.T

    :Results…………………………………………………....……………………………………

**B. OTHER FINDINGS AND COMMENTS**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**C. The bearer of this form has been examined and treated by;**

Name of the Dr. ………………………………………..Sign………………………………..

Date …………………………………………………… Stamp ………………………………

**D. PERSONAL HISTORY**

Has the examinee suffered from any of the following? If “YES” put a tick, if “NO” put “X”

Pneumonia ☐ Asthma ☐ Rheumatic fever ☐ Heart disease ☐

Anemia ☐ Operations serious accident ☐ cerebral malaria ☐

**NB:**

The school further asks to burden your kindness by stamping your official stamp on the photo affixed here by.

Thanking you in advance for your cooperation.